# Gugu Kongwa latishia ustawi wa malisho ya mifugo kanda ya kati

Na Mbaraka Kambona

WATAFITI kutoka ChuoKikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwa kushirikiana na Serikali, wamesema kunahaja ya kuchukua hatua za haraka kudhibiti kusambaa kwa mmea wa Gugu Kongwaambao umeonesha kuathiri kwa kiasi kikubwa maeneo ya malisho yaliyopo wilayaniKongwa na mkoani Singida.

Hayo yalibainishwa na wataalamuhao walipokutana na wadau wengine wa sekta ya mifugo jijini Dodoma Oktoba juzikuwasilisha matokeo ya awali ya utafiti waliofanya kujua tabia za ukuajina usambaaji wa mmea huo ili kutafuta njia fungamanishi za kupunguza aukutokomeza kabisa mmea huo ujulikanao Gugu Kongwa.

Akizingumza katika mkutanohuo, Mtafiti Kiongozi kutoka SUA, Dk. Selemani Ismail alisema utafiti wa GuguKongwa ulilenga kujua tabia ya ukuaji wake na kwa kiasi gani mmea huounaoathiri malisho ya mifugo umesambaa.

"Utafiti wa awalitulioufanya kwa miaka miwili (2), ulilenga kutafuta njia shirikishi zakupunguza au kuangamiza kabisa mmea huo wa Gugu Kongwa ambao usambaaji wakeumekuwa na athari kubwa katika maeneo mengi ya malisho hususan katika maeneo yaKanda ya Kati na Mkoa wa Manyara," alisema Dk. Ismail

Dk. Ismail aliendeleakusema kuwa katika kutafuta njia ya kudhibiti Gugu Kongwa, walifanya utafiti nakupata mmea unaoitwa Melia ambao umeonesha ufanisi katika kutokomeza usambaajiwa Gugu Kongwa.

Scanned with CamScanner

# Gugu Kongwa latishia ustawi wa malisho Kanda ya Kati

NA MWANDISHI WETU

WATAFITI kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwa kushirikiana na Serikali wamesema kuna haja ya kuchukua hatua za haraka za kudhibiti kusambaa kwa mmea wa Gugu Kongwa ambao umeonesha kuathiri kwa kiasi kikubwa maeneo ya malisho yaliyopo Wilayani Kongwa na Mkoani Singida.

Hayo yalibainishwa na Wataalamu hao walipokutana na wadau wengine wa Sekta ya mifugo jijini Dodoma Oktoba 22, 2021 kuwasilisha matokeo ya awali ya utafiti waliofanya kujua tabia za ukuaji na usambaaji wa mmea huo ili kutafuta njia fungamanishi za kupunguza au kutokomeza kabisa mmea huo ujulikanao Gugu Kongwa.

Akiongea katika Mkutano huo, Mtafiti Kiongozi kutoka SUA, Dkt. Selemani Ismail alisema utafiti wa Gugu Kongwa ulilenga kujua tabia ya ukuaji wake na kwa kiasi gani mmea huo unaoathiri malisho ya Mifugo umesambaa.

"Utafiti wa awali tulioufanya kwa miaka miwili (2) ulilenga kutafuta njia shirikishi za kupunguza au kuangamiza kabisa mmea huo wa Gugu Kongwa ambao usambaaji wake umekuawa na athari kubwa katika maeneo mengi ya malisho hususan katika maeneo ya Kanda ya Kati na Mkoa wa Manyara," alisema Dkt. Ismail

Dkt. Ismail aliendelea kusema kuwa katika kutafuta njia ya kudhibiti Gugu Kongwa walifanya utafiti na kupata mmea unaoitwa Melia ambao umeonesha ufanisi katika kutokomeza usambaaji wa Gugu Kongwa.

"Utafiti wetu tuliufanya Wilayani Kongwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ili kutokomeza mmea huo na kulinda malisho kwani likiachwa liendelee kusambaa athari zake ni kubwa sana kwa malisho ya mifugo," aliongeza

Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Kejeri Gillah alisema kuwa Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inajipanga kuhakikisha matokeo hayo ya utafiti yanakwenda kufanyiwa kazi.

"Tumeona athari kubwa za gugu hili vamizi katika maeneo yetu ya malisho na hivyo ni muhimu kulidhibiti mapema ili lisisababishe uhaba wa malisho na kupunguza tija katika uzalishaji," alisema Dkt. Gillah

Naye, Meneja wa Mfuko wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia kutoka COSTECH, Ntufye Mwakigonja alisema anaimani kuwa utafiti huo utatatua changamoto hiyo inayokabili malisho nchini huku akiongeza kuwa wao kama COSTECH wataendelea kushirikiana na watafiti hao ili kuhakikisha matokeo hayo yanafanyiwa kazi kwa manufaa ya Sekta ya mifugo nchini.

Aidha, Wadau wa Sekta ya Mifugo waliohudhuria mkutano huo walisema kuwa pamoja na kuwepo changamoto zinazosababishwa na mmea huo katika malisho ya mifugo, watafiti hao waendelee kufanya utafiti kuangalia mtizamo chanya ambao unaweza kusaidia jamii kutumia faida zinazoweza kupatikana zitokanazo na Gugu Kongwa.

Scanned with CamScanner

# Watafiti SUA waonya kuenea magugu kongwa

**Na Mbaraka Kambona**

WATAFITI kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamesema kuna haja ya kuchukua hatua za haraka kudhibiti kusambaa kwa mmea wa gugu kongwa ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa maeneo ya malisho ya mifugo wilayani Kongwa na mkoani Singida.

Wataalamu hao walitoa tahadhari hiyo walipokutana na wadau wa sekta ya mifugo jijini Dodoma kuwasilisha matokeo ya awali ya utafiti waliofanya kujua tabia za ukuaji na usambaaji wa mmea huo.

Mtafiti Kiongozi kutoka SUA, Dk Selemani Ismail alisema utafiti wa gugu kongwa ulilenga kujua tabia ya ukuaji wake na kwa kiasi gani unaoathiri malisho ya mifugo.

"Utafiti wa awali tulioufanya kwa miaka miwili ulilenga kutafuta njia shirikishi za kupunguza au kuangamiza kabisa mmea huo ambao usambaaji wake umekuwa na athari kubwa katika maeneo mengi ya malisho hususan katika maeneo ya Kanda ya Kati na mkoa wa Manyara," alisema.

Dk Ismail alisema katika kutafuta njia ya kudhibiti gugu kongwa, walifanya utafiti na kupata mmea unaoitwa melia ambao umeonesha ufanisi katika kutokomeza usambaaji wa gugu kongwa.

"Utafiti wetu tulifanya wilayani Kongwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri) na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ili kutokomeza mmea huo na kulinda malisho kwani likiachwa liendelee kusambaa athari zake ni kubwa sana kwa malisho ya mifugo," alisema.

Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Kejeri Gillah alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine inajipanga kuhakikisha matokeo hayo ya utafiti yanakwenda kufanyiwa kazi.

"Tumeona athari kubwa za gugu hili vamizi katika maeneo yetu ya malisho, hivyo ni muhimu kulidhibiti mapema ili lisisababishe uhaba wa malisho ya mifugo na kupunguza tija katika uzalishaji," alisema.

Meneja wa Mfuko wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia (Costech), Ntufye Mwakigonja alisema ana imani utafiti huo utatatua changamoto hiyo inayokabili malisho ya mifugo nchini.

Alisema Costech itaendelea kushirikiana na watafiti hao ili kuhakikisha matokeo hayo yanafanyiwa kazi kwa manufaa ya sekta ya mifugo nchini.

Wadau wa sekta ya mifugo waliohudhuria mkutano huo waliwataka watafiti hao waendelee kufanya tafiti kuangalia namna wanaweza kusaidia jamii kutumia faida zinazoweza kupatikana kutokana na gugu kongwa.

Scanned with CamScanner

# Sua, Serikali kuthibiti gugu kongwa

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Morogoro. Watafiti wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (Sua), kwa kushirikiana na Serikali wamesema kuna haja ya kuchukua hatua za haraka kudhibiti kusambaa kwa mmea wa gugu kongwa ambao umeonyesha kuathiri maeneo ya malisho wilayani Kongwa mkoani Dodoma na Singida.

Wataalamu hao walisema hayo jana walipokutana na wadau wa sekta ya mifugo kutoka Dodoma kwa lengo la kuwasilisha matokeo ya awali ya utafiti walioufanya.

Akizungumza katika mkutano huo, Mtafiti Kiongozi kutoka Sua, Dk Selemani Ismail alisema utafiti wa gugu kongwa ulilenga kujua tabia ya ukuaji wake na kwa kiasi gani unaathiri malisho ya mifugo.

"Utafiti wa awali tulioufanya kwa miaka miwili ulilenga kutafuta njia shirikishi za kupunguza au kuangamiza kabisa mmea huo ambao usambaaji wake umekuwa na athari kubwa katika maeneo mengi ya malisho hasa katika maeneo ya Kanda ya Kati na Mkoa wa Manyara," alisema Dk Ismail.

Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Kejeri Gillah alisema wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inajipanga kuhakikisha matokeo hayo ya utafiti yanakwenda kufanyiwa kazi.

Meneja wa Mfuko wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia kutoka Costech, Ntufye Mwakigonja alisema anaimani utafiti huo utatatua changamoto hiyo inayokabili malisho nchini.

"Tumeona athari kubwa za gugu hili vamizi katika maeneo yetu ya malisho, hivyo ni muhimu kulidhibiti mapema ili lisisababishe uhaba wa malisho na kupunguza tija katika uzalishaji."
Dk Kejeri Gillah

Scanned with CamScanner